

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
SHULE YA SEKONDARI NKOKASHU,  
S.L.P 6976,  
MOSHI.  
04/12/2020

Kumb.Na.NKSS/JIN/2021/VOL 01

Jina la Mwanafunzi.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI  
NKOKASHU WILAYA YA HAI, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.**

### **1.0 UTANGULIZI**

Nina furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Nkokashu mwaka 2021

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shulenii tarehe **11/01/2020** saa mbili asubuhi bila kukosa.

### **2.0 MAHITAJI MUHIMU YA SHULE.**

#### **a) Sare ya shule**

**Wavulana:** Shati mbili nyeupe na suruali mbili za rangi **DAMU YA MZEE (MAROON)** (**Kitambaa kimeambatanishwa**) upana wa suruali uwe inch 7. Rangi ya sweta ni **DAMU YA MZEE** Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi vyenye kamba visiwe **raba** na visiwe na kisigino kirefu na soksi pea mbili rangi nyeusi.

**Wasichana:** Blauzi mbili nyeupe na sketi mbili rangi **DAMU YA MZEE (MAROON)** (**Kitambaa kimeambatanishwa**) sketi iwe pana na urefu ufile chini ya goti Rangi ya hijab iwe ya rangi nyeupe. Rangi ya sweta iwe **DAMU YA MZEE(MAROON)**, viatu pea mbili vya ngozi vyenye kamba visiwe **raba** na visiwe na kisigino virefu na soksi pea mbili rangi nyeupe.

Sare ya michezo kwa shule hii ni jezi za rangi **BLUE** kwa wavulana na wasichana.

**NB MWANAFUNZI ATAKAYE SHONA SKETI NDEFU ZA KUFUNIKA VIATU HATAPOKELEWA SHULENI.**

**b) vifaa vya taaluma**

Daftari (COUNTER BOOK) 12 Quire 3, madaftari madogo tisa ya mazoezi, kalamu za bluu na mkebe wa hesabu (mathematical set), rula, penseli na ufuto. Begi imara la kubebia vifaa vya shule.

**Angalizo: Mzazi/mlezi umlete mwanao siku ya kuripoti shuleni akiwa na sare zote kwa idadi inayotakiwa na vifaa vya taaluma vyote ili vikaguliwe ili kuepuka usumbufu kwa mwanafunzi masomo yanapoanza. Mwanafunzi hatapokelewa bila mzazi na mahitaji yanayotakiwa.**

**c) UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA VIFAA VYA USAFI.**

Kaika kutunza mazingira ya shule mwanao anatakiwa kuja na **Ndoo, Slasher na fagio wa chelewa**

**d) Mwanafunzi aje na cheti cha kuzaliwa**

KUTAKUWA NA **KIKAO CHA WAZAZI** WOTE WA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA 2021 NKOKASHU SEKONDARI SIKU YA JUMATANO TAREHE **06/01/2021** SAA MBILI KAMILI ASUBUHI.

### **3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo kabla na baada ya kuripoti shulenii:

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation); ukiwa nyumbani.
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g) Kuvaas sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- i) Kutunza mali za umma, za wengine na zako binafsi.

### **3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi (ugoro)na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, ya mwenzako au ya kwako binafsi.
- g) Kudharau bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito au kusababisha mimba.
- i) Kuoa au kuolewa
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

### **4.0 MAMBO MUHIMU YA KUKAMILISHA**

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa Shulenii mara utakaporipoti shulenii.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na kutii sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

### **5.0 Tafadhali mzazi na mwanafunzi soma kwa makini maelezo na maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.**

HEADMASTER  
MOKASHUSEC.SCHOOL  
P.O.Box 6976 MOSHI

## AHADI YA UTII

### A. Ahadi ya mwanafunzi

Mimi .....nakubali kupokea nafasi hii ya masomo katika shule ya sekondari NKOKASHU niliyopewa na serikali.Naahidi kuwa mtii wa sheria zote za shule, nitakuwa mwaminifu, nitajitahidi kujifunza kwa bidii na kwa kadiri ya uwezo wangu na kufanya kazi nyinginezo nitakazopangiwa kwa juhudini na maarifa.

**NB:Kushindwa kwangu kutiia ahadi hii, kanuni na sheria za shule zichukue mkondo wake.**

Saini ya mwanafunzi.....

Anuani ya nyumbani.....  
.....

### A. Ahadi ya mzazi/mlezi

Mimi .....nimekubali kumpatia mwanangu (jina la mwanafunzi husika).....

Mahitaji yote muhimu ya shule (sare ya shule, madaftari, kalamu, vifaa vingine vitakavyohitajika shulenik) ili aweze kujifunza bila matatizo. Naahidi pia kushirikiana na walimu katika kumlea, kumhimiza kujifunza na kufuata sheria za shule, na kumhudumia kadiri ya uwezo wangu.

**NB:Kushindwa kwangu kutimiza ahadi hii, kanuni na sheria za nchi na za shule zichukue mkondo wake.**

Saini ya mzazi/mlezi.....

Anuani .....NAMBA YASIMU 1.....2.....

## NDUGU WA KARIBU KWA MAWASILIANO

1. JINA .....NAMBA YA SIMU.....

2. JINA .....NAMBA YA SIMU.....

3. JINA .....NAMBA YA SIMU.....

## SEHEMU UNAYOISHI MZAZI/MLEZI

KIJIJI CHA ..... KITONGOJI CHA.....

JINA LA M/KITI WA KIJIJI/.....KATA YA.....

**PRESIDENT'S OFFICE – RALG**  
**HAI DISTRICT COUNCIL**  
**NKOKASHU SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

*(This form should be filled by government medical officer)*

STUDENT FULL NAME.....

AGE .....

BLOOD COUNT (red and white).....

STOOL.....

URINE.....

V.D.....

T.B.....

EYES.....

EARs.....

TEETH.....

SKIN.....

TREATMENT GIVEN (if any).....

.....  
ABDOMEN.....

HEART.....

ANY ADDITIONAL INFORMATIONS e.g. Physical defect, infections, impairments and any other abnormalities.....  
.....  
.....

I certify that the above examinee is fit.

**SIGNATURE.....**

**NAME.....**

**DATE.....OFFICIAL STAMP.....**

